TUME YA KIKRISTO YA HUDUMA ZA JAMII
KAMATI YA MITIHANI YA PAMOJA KANDA YA KASKAZINI

MTIHANI WA UTAMIRIFU KIDATO CHA SITA, 2026

121/2 **KISWAHILI 2**

Muda: Saa 3 **Jumatatu, 2 Machi 2026 Mchana**

Maelekezo

1. Mtihani huu una **sehemu A na B,** zenye jumla ya **maswali nane (8)**
2. Jibu maswali yote katika sehemu **A** na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu **B**. swali la **tano (5)** ni la lazima.
3. Zingatia **maelekezo** ya **kila sehemu** na ya kila swali
4. Simu za **mkononi** na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (Alama 40)
Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. "Mhimili mkubwa ujengao fasihi andishi ni fasihi simulizi". Onesha mchango wa fasihi simulizi katika fasihi andishi. Kwa kutoa hoja **tano** na mifano.

2. "Fasihi simulizi huchomoza katika jamii ambayo huandamwa na mabadiliko mbalimbali". Thibitisha dai hili kwa kutumia hoja **tano** ukionesha mabadiliko ya uhifadhi wa fasihi simulizi,

3. Ujio wa wazungu nchini Tanzania umechangia maendeleo ya tamthiliya ya Kiswahili. Kwa kutumia mifano zifafanue aina **tano** za tamthiliya ya Kiswahili.

4. Soma habari ifuatayo kisha eleza mbinu za kifani zilizotumika.

   Nilipomwona kwa mara ya kwanza nilimwelewa sivyo ndivyo. Kuwa mwanamali mchanga ambaye ndiye kwanza alfajiri yake inachipua kulichofanya nimwelewe anavyotakiwa kueleweka harimu ya aina yake. Kwa kufungua ukurasa wa maisha yake hivi karibuni tu, ni kwa mengi yaliyojaa wingi wa mama dunia hajakutana nayo maishani.

   Ikrani, sikuwa na kosa kuamini nilivyoamini maana umri wake kwa kumwangalia tu ulionesha kutokupindukia miaka kumi na miwili. Kwa kawaida umri huu ni wa amani na furaha nyingi kwa wana wengi wa Baba Adam na Mama Hawa. Kama si uzembe wa wazazi au walezi mtoto huwa kati ya pepo ambayo wengi huja kuijutia ukubwani. Ni umri wa mkono kwenda kinywani bila kujua kilichotiwa kinywani kinatoka wapi; ni umri wa kununa na kulia nukta hii, kisha ukatabasamu na kucheka nukta hiyo, ni umri wa kuwa na almasi mkononi, ukaridhia kutupa ili uokote peremende.

   Hatua zake hazinishughulishi sana maana kama nilivyosema awali katika umri huu wa ujana kuyumba hivi anavyoyumba ni sehemu ya maisha na mtu aliyekula chumvi nyingi kiasi kama mimi si jambo la kuajabia hata kidogo aina ya mwendo huu. Hii hatua yake kunijia hapa nilipoketi pia hainishtushi maana anaweza kuja na mengi tu, mfano, kuomba au kuuliza juu ya kitu Fulani na kitu kama hicho.

   Vipi mshikaji mambo? Yanamtoka maneno haya mara tu anapofika. Aina ya salamu yake inaifanya kengele yangu ya tahadhari ipige kelele huko ubongoni. Kabla sijaupata ulimi wangu kujibu salamu yake yeye tayari kaketi hapa kando yangu na kuvuta gazeti nililoshika mkononi nikilisoma na kulitia majapani mwake mithili ya mtu anayejiandaa kusoma au kitu kama hicho, lakini hafanyi hivyo bali anamgeukia huku kachanua tabasamu na kutamka kwa mbwembwe, nimekuona kitambo kiasi…… nikaona nije niungane nawe. Navutiwa kukuona hivi…… napenda kuwa karibu nawe …….
   Tayari nimeupata ulimi wangu na nimeirejesha salamu yake ila hayo maelezo aliyoyatoa hivi punde yamenichanganya. Kwa kuwa sioni cha maana kutia kwenye kauli yake ya kutatanisha, natabasamu na kuendelea kumtazama tu. Yeye wala hana wasiwasi ananitazama kwa uhakika kisha anarejesha macho katika gazeti alilolitandaza mapajani kwake ambapo namuona analipekua. Anaendelea kufanya hivyo mpaka anafikia ukurasa huo aambao una makala ya jamii.namuona anasita kwa muda kabla ya kumtupa swali hili. Umesoma hapa?

Ukurasa wa 2 kati ya 3

Swali lake hili kiasi limenigutusha na kufanya niyatupe macho yangu kwa bidii kwenye hiyo makala ananionesha. Hapa nakutana na kichwa kinasema "Tamtam ya Huba". Nayadondosha macho huko na kumtazama kwa mshangao huku nikiguna kimoyomoyo kabla sijasoma……. Nalazimika kushusha pazia la ngano hapa kwa miradi ya kuendelea na ngano hii tutakapokutana mara nyingine.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka katika sehemu hii. Swali la **tano (5)** ni la lazima

5. Uteuzi mzuri wa mandhari ni kielelezo cha kufanikiwa kwa mwandishi. Thibitisha kauli hii kwa kutumia diwani mbili ulizosoma. Hoja **nne (4)** kwa kila diwani.

6. "Watunzi wa ushairi huwa na dhima anuai kwa jamii katika kazi zao wanazotunga." Kwa kutumia diwani mbili ulizosoma, tathmini kauli hiyo kwa kutoa hoja **tatu (3)** kwa kila diwani.

7. Uhuru wowote usipowekewa mipaka unaweza kugeuka na kuwa janga na kusababisha madhara katika jamii. Kwa kutumia riwaya mbili ulizosoma onesha ukweli wa kauli hiyo. Hoja **nne (4)** kwa kila kitabu.

8. Fikra zenye kuleta mabadiliko ya haraka huhitajika katika kuondoa utendaji mbovu katika jamii. Jadili kauli hii kwa kutoa hoja **nne (4)** kwa kila kitabu katika tamthiliya mbili ulizosoma darasani.

ORODHA YA VITABU

USHAIRI

Kimbunga	-	Haji Gora
Mapenzi Bora	-	Shabani Robert
Chungu Tamu	-	Theobald A. Mvungi
Fungate ya Uhuru	-	Mohamed S. Khatibu

RIWAYA

Usiku utakapokwisha	-	Mbunda Msokile
Kufikirika	-	Shabani Robert
Mfadhili	-	Hussein Tuwa
Vuta N'kuvute	-	Shafi Adama Shafi

TAMTHILIYA

Kwenye Ukingo wa Thim	-	Ebrahim Hussein
Morani	-	Emmanuel Mbogo
Kivuli Kinaishi	-	Said Mohamed
Nguzo Mama	-	Penina Muhando